3. Wadau mbalimbali watakaoguswa na huduma na hivyo kuamua kuchangia kwa hiyari yao wenyewe.

Michango yote ya huduma hukusanywa kupitia:

Nambari ya akaunti ya benki ***20110077511***

Jina la Akaunti ***Tujenge Nyumba ya Mungu***

Jina la Benki ***NMB*** katika tawi la ***Bank House***

# Mafanikio ya Huduma

Tunamshukuru Mungu kwa jinsi ambavyo amekuwa nasi katika huduma hii kwani mbali na kanisa lililojengwa ***Wilayani Bunda Mkoani Mara mnano mwaka 2021***, hadi sasa tangu huduma ilipowekwa wakifu mwezi Machi, 2023, tumefanikiwa kukamilisha ujenzi wa makanisa kumi na mbili (12). Makanisa hayo yamejengwa katika mikoa ya Lindi na Mtwara kama ifuatavyo: katika mkoa wa **Mtwara** tumejenga makanisa **tisa (9)** katika eneo la ***Mitengo Wilayani Mtwara***, katika vijiji vya ***Hinju na Nanjedya Wilayani Nanyamba,*** *katika vijiji vya* ***Ngunja, Mahoha, Mambamba, Lienje na Mdimba*** *Wilayani* ***Tandahimba***. Katika mkoa wa **Lindi** tumejenga makanisa **matatu (3)** kama ifuatavyo: katika kijiji cha **Mpiruka, Namikango na Lionja B** Wilayani **Nachingwea**.
Wakati huo huo ndani ya mwaka huu 2025, tunayo mipango ya kukamilisha ujenzi wa makanisa ***mawili*** katika vijiji vya **Mtualonga** na **Kiwalala** huko Wilayani ***Mtama***. Pia katika mwaka huu wa 2025, tumepanga kuanza na kukamilisha ujenzi wa ***majengo manne (4)*** *ya makanisa katika vijiji vya* ***Namtumbuka*** *Wilayani* ***Nanyamba, Mihambwe*** *Wilayani* ***Tandahimba, Miyuyu*** *Wilayani* ***Newala*** *na kijiji cha* ***Moma-Kitama*** *Wilayani* ***Mtwara Vijijini***.

## Sifa za Mshirika

Mtu yeyote anaweza kuwa mshirika wa huduma hii ilimradi awe na sifa zifuatazo:

- Awe tayari kuchangia rasilimali zake ili kufanikisha malengo ya huduma